Unasikia Vizuri Kiasi Gani?

(How Well Do You Listen?

Na

Ellis P. Forsman

Unasikia Vizuri Kiasi Gani?

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

Unasikia Vizuri Kiasi Gani?

Mat. 11:15

Wakati wa huduma yake duniani, mara nyingi Yesu alihitimisha somo kwa kulia, "*Yeye aliye na sikio, na asikie!*"

- Kuhusu Yohana Mbatizaji. Mat. 11:15, "*Mwenye sikio, na asikie.*"
- Kuhusu mfano wa mpanzi. Mat. 13:9, "*Aliye na sikio, na asikie.*"
- Kuhusu maelezo ya mpanzi wa mbegu. Mat. 13:43, "*Ndipo wenye haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Mwenye masikio nja asikie*."

Katika barua yake kwa makanisa ya Asia, Yesu alihitimisha kila barua kwa neno linalofanana: "*Yeye aliye na sikio na asikie ambacho Roho ayaambia makanisa…*" (Ufu. 2:7; Ufu. 2:11; Ufu. 2:17; Ufu. 2:29; Ufu. 3:6; Ufu. 3:13; & Ufu. 3:22).

Kuna maantiki gani katika misemo hii?

Ni kama kusema "*Kinachosemwa ni muhimu sana, hivyo ni heri usikilize kwa makini!*"

Marko 4:23-25, "*Mtu akiwa na masikio ya kusikilia, na asikie. Akawaambia angalieni msikialo; kipimo kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa, na tena mtazidishiwa. Kwa maana mwenye kitu atapewa, na asiye na kitu hata kile alicho nacho atanyang'anywa.*"

Inaonyesha kwamba Yesu alikuwa na shida ambayo ipo hata leo.

Watu wengi hawasikii, au hawasikii ili waelewe.

Ninashawishika kwamba wengi leo hawashukuru umuhimu wa kusikia vizuri. Yesu alijali sana.

Hivyo ni jukumu sahihi kuuliza, "Unasikia Vizuri Kiasi Gani?" Inaweza kuwa na faida kuanza na kuzionyesha:

Aina tatu za wasikivu

"Kiziwi wa kusikia".

Baadhi ya Wakristo wa Kiebrania walikuwa hivi. Heb. 5:11, "*Ambaye tuna maneno mengi ya kunena katika habari zake; na ni shida kuyaeleza kwa kuwa mmekuwa wavivu wa kusikia.*"

Angalia kwamba mtu anapokuwa na tatizo hili, inakuwa vigumu kwa watu kuwaambia vitu! Kosa haliko katika "somo" maandishi, au "mtoa somo", bali tatizo liko kwa "msikiaji"!

Isaya aliandika kuhusu watu hao, na Yesu akaliongelea kwa wengi katika siku zake duniani. Mat. 13:13-15, "*Kwa sababu hii nasema nao kwa mifano; kwa kuwa wakitazama hawaoni, na wakisikia hawasikii, wala kuelewa. Na neno la nabii Isaya linatimia kwao, likisema, kusikia mtasikia wala hamtaelewa; kutazama mtatazaama wala hamtaona. Maana mioyo ya watu hawa imekuwa mizito, na kwa masikio yao hawasikii vema, na macho yao wameyafumba; wasije wakaona kwa macho yao, wakasikia kwa masikio yao, wakaelewa kwa mioyo yao, wakaongoka nikawaponya.*"

Watu wako hivi kwa sababu ni viziwi katika mioyo! Hii inawazuia katika:

- Kuelewa ukweli wa Mungu.
- Kuacha dhambi na kumgeukia Mungu.
- Na kuokolewa na Mungu!

Ni nani angependa kuwa msikivu wa aina hii?

Wale walio na "masikio yenye utafiti".

Paulo anaeleza haya katika 2 Tim. 4:3-4, "*Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.*"

Watu kama hao husikia tu yale wanayopenda kusikia…

Hivyo hawapendi "mafundisho yenye uzima" (ambayo mara nyingu uhitaji aina ya mahubiri inayoelezwa katika: 2 Tim.4:2, "*Lihubiri neno uwe tayari, wakati ukufaao na wakati usiokufaa, karipia, kemea, na kuonya kwa uvumilivu wote na mafundisho.*"

Watawatafuta waalimu wanaowapenda…lakini wataacha ukweli na kugeukia hadithi. Wengi leo hujikwa kwa hili tatizo la "kusikia!"

Wale wanaosikia kwa "wema na mioyo mizuri".

Yesu anawaongelea watu hawa katika Luka 8:15, "*Na zile penye udongo mzuri, ndio wale ambao kwa unyofu wa mioyo yao hulisikia neno, na kulishika; kisha huzaa matunda kwa uvumilivu.*"

Waberoya walikuwa wasikivu wa aina hii. Mdo. 17:11, "*Watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwa kuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo.*"

Walikuwa "wanyofu wa moyo" (NKJV), hivyo walikuwa tayari kumpa Paulo usikivu mzuri. Ilionyesha ni jinsi gani "walivyopokea" (au kusikia) neno: "kwa utayari wote".

Huu ndio usikivu tunaopaswa kuwa nao!

Kwa nini ni muhimu kuwa aina hii ya wasikiaji? Kuna sababu aina nyingi:

Umuhimu wa msikivu mzuri

Umuhimu wa kubarikiwa.

Kwa wale wanaopenda kusikilizaa, kuna vitu vizuri vya kujifunza. Mat. 13:16-17, "*Laakini hri macho yenu kwa kuwa yanaona; masikio yenu kwa kuwa yanasikia. Kwa maana amini nawaambia, manabii wengi na wenye haki walitamani kuyaona mnayoyaona ninyi, wasiyaone; na kuyasikia mnayoyasikia ninyi, wasiyasikie.*"

Vitu vingi ambavyo watu wakuu (Daudi, Danieli, n.k) hawakupata nafasi ya kujifunza. Vitu vinavyoendana na baraka za ajabu ambazo zipo sasa ndani ya Kristo!

Efe. 1:3, "*Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni katika ulimwengu wa Roho ndani yake Kristo.*"

Tunaweza kuzikosa baraka hizi iwapo hatusikii kwa umakini.

Ni muhimu katikaa imani inayookoa.

Mungu amechagua kwamba tuokolewe kupitia imani katika Kristo. Rum. 1:16-17, "*Kwa maana siionei haya injili kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye kwa Myunani kwanza, na kwa Myahudi pia. Kwa maana haki ya Mungu inadhihirishwa ndani yake, toka imani hata imani kama ilivyoandikwa, mwenye haki ataishi kwa imani.*"

Imani kama hiyo huja kupitia kuhubiri injili, mara nyingi inahusisha kumsikiliza mhubiri.

- Rum. 10:14, "*Basi wamwiteje yeye wasiyemwamini? Tena wamwaminije yeye wasiyemsikia? Tena wamsikieje pasipo mhubiri?*"
- Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Wakati mtu mwingine anaweza kuwa na imani kwa kusoma neno la Mungu (Yohana 20:30-31), ukweli unabaki kwamba wengi mara nyingi ni tegemezi ya kile wanachokisia kinatangazwa kwa amara ya kwanza.

Yohana 20:30-31, "*Basi kuna ishara nyingine nyingi alizozifanya Yesu mbele ya wanafunzi wake zisizoandikwa katika kitabu hiki. Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo Mwana wa Mungu; na kwa kuamini mwe na uzima kwa jina lake.*"

Kinachosababisha imani inakosekana ni kwa sababu watu sio wasikivu wazuri. Wanaacha ushahidi wa neno la Mungu ambao unaaleta imani!

Je usikivu wako unazuiaa maendeleo ya imani yako?

Muhimu katika kuzaa matunda.

Katika mfano wa mpanzi, aina pekee (moyo) unaoweza kuzaa matunda ulikuwa ni ule uliosikiliza vyema. Luka 8:15, "*Na zile penye udongo mzuri ndio wale ambao kwa unyofu na wema wa mioyo yao hulisikia neno na kulishika; kisha huzaa matunda kwa uvumilivu.*"

Hiyo ni kwa sababu kuzaa matunda huja kutokana na "kuelewa" neema ya Mungu! Kol. 1:6, "*Iliyofika kwenu, kama ilivyo katika ulimwengu wote, na kuzaa matunda na kukua kama inavyokuwa kwenu pia, tangu siku mlipoisikia na mkaifahamu sana neema ya Mungu katika kweli;*"

Kumbuka kwamba injili ilikuwa inazaa matunda kwa Wakolosai. Lakini hiyo ilikuwa ni "*tangu siku mlipoisikia na kufahamu sana neema ya Mungu katika kweli.*"

Ni kwa kusikiliza vizuri ndivyo tunawezaa "kuelewa" neema ya Mungu na hivyo kutoa motisha kuzaa matunda katika utukufu wake!

Muhimu katika kuzuia upotofu (kuanguka).

Kuna hatari ya kupotoka, kwa kukataa "wokovu mkuu"

Heb. 2:1-3, "*Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosa. Kwa maana ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki, sisi je! Tutapataje kupona tusipojali wokovu mkuuu namna hii? Ambao kwanzaa ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia;*"

Suluhisho pekee ni "kuwa makini katika kusikia kwetu".

Usikivu mbaya siku zote ni hatua ya kwanza mbaya katika kupotoka!

Muhimu katika kukwepa kukataliwa na hukumu.

Kama tusiposikia, tunavyopaswa, tunajihukumu wenyewe kwamba hatufai katika uzima wa milele.

Mdo. 13:44-49, "*Hata sabato ya pili watu wengi karibu mji wote wakakusanyika walisikie neno la Mungu. Bali Wayahudi walipowaona makutano wakajaa wivu wakayakanusha maneno yaliyonenwa na Paulo, wakibisha na kutukana. Paulo na Barnaba wakanena kwa ushujaa wakasema, ilikuwa lazima neno la Mungu linenwe kwenu kwanza; lakini kwa kuwa mnalisukumia mbali na kujiona nafsi zetu kuwa hamkustahili uzima wa milele, angalieni twawageukia Mataifa. Kwa sababu ndivyo tulivyoamriwa na Bwana, nimekuweka uwe nuru ya mataifa, upate kuwa wokovu hata mwisho wa dunia. Mataifa waliposikia hayo wakafurahi, wakalitukuza neno la Bwana, nao waliokuwa wamekusudiwa uzima wa milele wakaamini. Neno la Bwana likaenea katika nchi ile yote.*"

Kama tukikataa injili (labda kwa usikivu mbaya?), basi watu wa Ninawi na Malkia wa kushi watatuhukumu siku ya hukumu!

Mat. 12:41-42, "*Watu wa ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu wao walitubu kwa mahubiri ya Yona na hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona. Malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa; kwa sababu yeye alikuja pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani na hapa yupo aliyemkuu kuliko Sulemani*."

Watu wa Ninawi wakatubu baada ya kusikia somo moja tu kutoka kwa Yona; tunaweza kukataa injili ya Kristo baada ya kupewa nafasi nyingi?

Malkia wa kusini aliendelea zaidi kussikiliza hekima ya Sulemani; tunapenda kwend japo hatua kidogo kusikia hekima ya neno la Mungu ikitangazwa.

Kukataliwa na hukumu hauishii tu kuja kwa hawa wachache tu…itatoka kwa Mungu pia!

Natarajia, tunashukuru kwa nafasi nzuri tuliyonayo kwamba tunaweza kusikiliza neno la Munguna umuhimu wa usikivu mzuri! Tunawezaje kuwa na maendeleo ya usikivu mzuri? Maana kama mnenaji tunapaswa kujifunza kuongea na kuelewa, watu wanapaswa kujifunzaa kusikia kama kuelewa! Hapa kuna baadhi…

Hatua za usikivu bora

Fanya usikivu kuwa tendo la ibada.

Jinsi unavyosikiliza neno la Mungu ikisomwa au kuhubiriwa ni ishara zaidi ya kujitoa kwako kwa Mungu kama unavyoomba au kuimba.

Hivyo ukiwa na nafasi ya kusikia, fanya hivyo kwa "nia ya kuabudu". Fikiria jinssi utakavyosikiliza kama mtu mkubwa angekuwa anaongea. Ebu fikiria umakini wako kama ungekuwa unamsikiliza mtu maarufu.

Kutangazwa kwa neno la Mungu si kunafaa kuwa na umakini zaidi?

Sikiliza kwanzia mwanzo hadi mwisho.

Kuwa na usikivu mwanzo mwisho. Unatarajia kuelewa hadithi kirahisi kwa kusoma sentensi hapa na pale? Hivyo ni katika kusikia… sentensi, neno, misemo, neno ambayo inafaa kueleweka lazima isikikie kulingana na mazingira inayozungumzwa.

Msemaji lazima afuate miongozo fulani ya kunena ili aweze kueleweka:

- Utangulizi wa somo.
- Wakilisha neno kuu kwa kusaidiwa na mabishano yaliyo na maantiki.

- Hitimisha kwa mukhtasari.

Msikilizaji lazima asikilize sehemu ZOTE ili kuelewa vyema.

Muangalie mnenaji au andika.

Hii inasaidia umakini wako. Ukiangalia sehemu nyingine inakuwa rahisi kufanya akili yako isitulie. Kufumba macho pia hukurahisisha kuweza kutoka kwenye msitari.

Hii inahitaji nidhamu ya kipekee, lakini inafaa kutengeneza umakini wa muda mrefu.

Ijaribu kuona kama inaleta tofauti!

Soma pamoja na Biblia yako.

Unakumbuka zaidi ya kile mnachosikia na kuona juu ya kile mnachosikia; ndiyo maana misaada ya kuona hutumika katika hotuba. Lakini msaada mkuu wa kuona ni Biblia yako!

Hekima yako ya kimaandiko itakuwa vizuri kwa kufanya hiki.

Ni vigumu mara ya kwanza kuwa macho lakini baadae itakuwa rahisi. Tunawahimiza watoto wetu kufanya hili, watu wazima hawapaswi kutoa mifano na kufanya vivyo hivyo?

Sikiliza kwa imani.

Sikiliza kwa utayari wa kukubali na kuamini kinachoonyeshwa katika neno la Mungu.

Angalia Heb. 4:1-2, "*Basi ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope mmoja wenu asije akaonekana ameikosa. Maana ni kweli sisi nasi tumehubiriwa habari njema vile vile kama hao. Lakini neno lile lililosikiwa halikuwafaa hao kwa sababu halikuchanganyika na imani ndani yao waliosikia.*"

Kama tusiposikiliza "kwa imani", vitu kama hivyo vitatutokea; i.e., kuanguka kutoka katika pumziko la mbingu.

Sikilizaa kwa nia ya kufanya tendo.

Je tunafafana na watu wa nyakati za Ezekieli? Eze. 33:30-32, "*Nawe mwanadamu wana wa watu wako wana wa watu wako husimulia habari zako karibu na kuta, na ndani ya milango ya nyumba zao, na kuambiana kila mtu na ndugu yake, wakisema haya twende tukasikie ni neno gani hilo litokalo kwa BWANA. nao huja kwako kama watu wajavyo, nao hukaa mbele yako kama watu wangu,, nao husikia maneno yako wasitende; maana kwa vinywa vyao hujifanya kuwa wenye upendo mwingi, lakini mioyo yao inatafuta faida yao. Na tazama wewe umekuwa kwao kama wimbo mzuri sana, wa mtu mwenye sauti ipendezayo, awezaye kupiga kinanda vizuri; maana wasikia maneno yako, lakini hawayatendi.*"

Walipenda kumsikia, lakini kwa nia mbaya. Je tunapenda kusikiliza hotuba kwa sababu ya anenavyo msemaji?

Kusikiliza lazima kusindikizwe na kutenda ili kuwe na faida. Yakobo 1:22-25, "*Lakini iweni watendaji wa neno wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa ni msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji, mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo asiwe msikiaji msahaulifu bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*"

Kama ilivyo muhimu kama msikiaji mzuri, baraka huja tu tukiwa wasikiaji na watendaji!

Hitimisho

Kuweza kubarikiwa katika kile nifanyalo hilo ndio lengo langu katika kutoa mawazo yangu haya katika kusikiliza, maana yote huanza na kusikilia kwa njia sahihi.

Hivyo usikivu ni muhimu kiasi gani?

Inapokuja kumsikiliza Mungu ni muhimu!

Isa. 55: 2-3, "*Kwani kutoa fedha kwa ajili ya kitu ambacho si chakula? Na mapato yenu kwa kitu kisichoshibisha? Nisikilizeni kwa bidii mpate kula kilicho chema, na kujifurahisha nafsi zenu kwa unono. Tegeni masikio yenu na kunijia; sikieni na nafsi zenu zitaishi; nami nitafanya nanyi agano la milele, naama rehema za Daudi zilizo imara.*"

Ni muhimu kwa uzuri wa nafsi zetu!

Je kuna wakati ambao MUNGU hakusikia kabisa?

Ndiyo, wakati dhambi zetu ni katika ya Mungu na sisi. Isa. 59:1-2, "*Tazama mkono wa BWANA haukupunguka hata usiweze kuokoa wala sikio lake si zito, hata lisiweze kusikia; lakini maovu yenu yamawafarikisha ninyi na Mungu wenu, na dhambi zenu zimeufichaa uso wake msiuone, hata hataki kusikia.*"

Lakini tunaweza kuwa makini na hilo tatizo la kupokea Rehema za Mungu. Isa. 55:6-7, "*Mtafuteni BWANA maadamu anapatikana, mwiteni maadaamu yu karibu; mtu mbaya na aache njia yake, na mtu asiye haki na aache mawazo yake; na amrudie BWANA naye atamrehemu; na arejee kwa Mungu wetu, naye atamsamehe kabisa.*"

Leo rehema hiyo inatolewa kupitia Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Na kama Mungu alivyosema katika Luka 9:35, "*...Huyu ni Mwanangu mpedwa: msikilize.*"

Je umemsikiliza kwa kutii neno lake? Au kilio hiki cha Yesu unakuhusu? Luka 6:46, "*Kwa nini mnaniita Bwana, Bwana, wakati hamtendi niwaambiayo?*"

Hatakusiliza isipokuwa umefanyika Mkristo? Zifuatazo ni hatua muhimu za kukufanya uwe Mkristo:

- **Imani.** Waeb. 11:6, "Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu, umri sawa na wa kwangu alikuwa haamini kuwa Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye ana kwa ana kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ili kuwa ni nzuri. Lakini ili kuwa upande ambao ni salama, labda anaweza kwenda kanisani, na kama akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri na kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "mambo haya hayafanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima umwamini yeye kwa moyo wako wote, la sivyo huwezi kumpendeza."
- **Toba.** Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

Matend. 11:18, "..... *Mungu amewapa pia mataifa toba liletalo uzima.*" Kama ulikuwa una lala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani humu!" unachukuwa simu na taratibu unawapigia polisi, ukiwambia kwamba kuna mwizi ndani kwako, na unawapa anwani ya nyumba yako. Kidogo, unawasikia wanafika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena na anataka kubadilisha maisha yake ili kwamba asiibe tena. Ni badiliko la akili linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kukifanya kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Warumi 10:9-10*, "Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hatakupata haki, na kwa kinywa hukiri hatakupata wokovu."*

Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu. Kumbuka kwamba katika somo hilo hapo juu imani (kuamini), toba na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" humaanisha kuelekea kitu fulani; si kwamba mtu tayari ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ndipo haki inapatikana, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote,

"*Lakini Yohana alitakakumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa alipanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa mpendwa wangu ninayependezwa*

naye." (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi ya kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia alisema "*imekuwa kwetu **sisi** kuitimiza haki yote."* Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, tusipobatizwa, bado tupo katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, tubuni makabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, ulisema ubatizo ni kwa ajili ya nini? *"Kwa ajili ya ondoleo la dhambi."* Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. *"Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye **na** kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Sasa unakawilia nini? Simama, ukabatizwe uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16).

Ubatizo ni agizo lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Hivyo mnazikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kama vile Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale ni lazima ufe. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaungana kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."* (Rum. 6:3-6).

Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa njia ya ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hapo juu inasema ubatizo ni maziko. Hatuendi makaburini na kuchukua udongo kidogo na kuweka juu ya mwili wa marehemu.

Kama hujafanyika mshiriki wa kanisa la Kristo, kwa nini usizingatie leo?

Ikiwa Watu Wengi Wanafanya Jambo, Je Hiyo Inathibitisha Kwamba Wanachofanya Ni Sahihi?